UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 08 Oktoba, 2022

Dorothea Chale

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi

TAMU TUME

MZUNGUKO WA UCHAGUZI

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limeanzishwa chini ya Ibara ya 5(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Kifungu cha 15B(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Tangu kuanzishwa kwa Tume, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limetumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Kwa mujibu wa Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na mambo mengine inawajibika:-

(i) Kusimamia na kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura wapya waliotimiza umri wa kuandikishwa; na

(ii) Kusimamia na kuratibu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Wajibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 15 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 21 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili, baada ya Uchaguzi Mkuu uliomalizika na kabla Uchaguzi Mkuu mwingine unaofuatia.

Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi yapata Wakurugenzi wapya

Na Mwandishi wetu

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Dkt. Wilson Mahera Charles amemteua Bi Dorothea Chale kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi kuanzia tarehe 17 Agosti, 2022 ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Mhe.Jaji Hamidu Mwanga ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Kabla ya uteuzi huo, Bi Dorothea alikuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi.

Kadhalika, Dkt. Mahera amemteua Bw. Kassim Sapi Mkwawa kuwa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi kuchukua nafasi ya Bi Dorothea Chale ambaye ameteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi.

Kabla ya uteuzi huo, Bw. Mkwawa alikuwa ni Afisa Sheria Mkuu Daraja la Kwanza kutoka Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi.

Dorothea Chale
Kaimu Mkurugenzi
Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na Raslimali Watu (Sehemu ya Raslimali Watu) Bw. Leonard Tumua, Dkt. Mahera amefanya uteuzi huo kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, kifungu Na. 6 (1) (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Wakati huo huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga kura (Habari), Dkt. Cosmas Mwaisobwa ni miongoni mwa watu saba walioteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

Taarifa iliyotolewa na Shirika hilo hivi karibuni, imewataja wajumbe wengine wanaounda bodi hiyo kuwa ni Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Bi. Tuma Abdallah, Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mtangazaji wa zamani wa Shirika hilo Bi. Amina Mollel, Bw. Innocent Mungy na Bi. Mwanjaa Lyezia.

Wengine ni Dkt. Hidelbrand Shayo pamoja na Mkurugenzi wa Mfuko wa Mawasiliano Tanzania, Bi. Justina Mashiba.

Kassim Sapi Mkwawa
Mkurugenzi Msaidizi
Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi

UNDP Yatembelea Tume ya taifa ya Uchaguzi

Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt.Wilson Mahera Charles (Katikati), Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo Duniani (UNDP), Bi.Christine Musisi (Kushoto) na Mkurugenzi wa Miradi na Sera kutoka UNDP Tanzania, Bw.Amon Manyama (Kulia), walipokuwa katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jijini Dodoma.

Mchakato wa kuanzisha Uchaguzi SACCOS wakaribia kukamilika

Na Mwandishi wetu

Mchakato wa kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo cha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Uchaguzi SACCOS LTD) unakaribia kukamilika baada ya wanachama wa chama hicho kupitia na kupitisha masharti ya chama, sera za mikopo, utumishi na uhasibu kabla ya kuziwasilisha kwa Mrajis wa Ushirika.

Akizungumza wakati wa mkutano wa pili wa wanachama kuelekea uanzishwaji wa Saccos hiyo uliofanyika katika Ofisi za Tume zilizopo Njedengwa jijini Dodoma, Afisa Ushirika wa Jiji la Dodoma Bw. Yusuph Richard amewataka viongozi na wanachama

kukamilisha taratibu zinazotakiwa na Mrajis ili Saccos hiyo iweze kuanza mapema iwezekanavyo.

Bw. Richard amesema ikiwa usajili utakubaliwa Uchaguzi Saccos itawakomboa wanachama wake kwa kujenga uchumi, kupata suluhisho la mtaji na kujenga familia zenye furaha.

“Hivyo tutumie nafasi hii kujadili yaliyomo kwenye katiba ya chama, sera ya mikopo, taratibu za ukopaji na taratibu za kusimamia fedha na sera ya utumishi, kwani ni lazima kwenye masuala ya fedha kuwepo na taratibu za kusimamia fedha hizo,” amesisitiza Bw. Richard.

Afisa Ushirika huyo ametaja baadhi ya vigezo vinavyotumika ili Saccos iweze kusajiliwa ambavyo kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2018 na 2013 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Namba 10 ya mwaka 2018, ni lazima Saccos ianze na mtaji usiopungua shilingi milioni 10 na kuendelea.

Kadhalika, ameongeza kuwa sera ya utumishi inatamka kuwa ni lazima Saccos ziwe na watendaji wake watakaosimamia ili kuwawezesha kuendesha chama hicho kwa mafanikio kama inavyoelekezwa na Sheria Namba 10 ya Huduma za Fedha.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya kuanzisha Uchaguzi Saccos Ltd Bw. Sosthenes Ngopa alimhakikishia Afisa Ushirika huyo kuwa kukamilisha taratibu zinazotakiwa kama alivyoelekeza kwa wakati ili mchakato wa kuanzisha saccos hiyo ukamilike mapema

Katika mkutano huo wa pili wa wanachama kuelekea uanzishwaji wa Uchaguzi Saccos wajumbe walipata fursa ya kutoa mawazo yao ili kuboresha sera ya mikopo na masharti ya chama hicho ambacho kinatarajiwa kuwa na wanachama 200 wa taasisi hiyo.

Kwa mujibu wa rasimu ya masharti (katiba) ya chama hicho, kujiunga kwa mwanachama mpya ambaye ni lazima awe mtumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kiingilio ni shilingi 50,000 na atapaswa anunue hisa 10 ambazo ni sawa na shilingi 100,000 pamoja na makato ya kila mwezi yanayoanzia shilingi 30,000 ambayo ni akiba yake.

NEC yatembelea vyombo vya habari kutoa elimu ya Mpiga Kura

Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura Monica Mnanka akifafanua jambo kwa wasikilizaji wa Radio Magic FM

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya ziara ya kutembelea vyombo mbalimbali vya habari na kuelimisha wananchi kuhusu majukumu ya Tume ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu endelevu la kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Ziara hiyo imefanyika Septemba mwaka huu ambapo Mkurugenzi Msaidizi (Elimu ya Mpiga Kura), Bi. Monica Mnanka ametembelea kituo cha televisheni cha Channel Ten, kituo cha redio cha Magic FM na Uhuru Radio na kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Bi. Mnanka amesema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 kifungu cha 4 C, Tume imepewa mamlaka ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura na kuratibu na kusimamia asasi zilizopewa kibali cha kutoa elimu hiyo.

“Tumeanza kutoa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari lengo likiwa ni kutekeleza jukumu la kutoa elimu endelevu ya mpiga kura ili wananchi wafahamu majukumu ya Tume,” amesema Bi. Mnanka na kufafanua kuwa;

“Wananchi wanatakiwa kufahamu sheria zinazoipa mamlaka Tume kutekeleza majukumu mbalimbali, mipaka ya Tume katika kutekeleza majukumu yake na jinsi Tume inavyoshirikisha wadau katika kutekeleza majukumu yake ya uchaguzi.”

Akizungumza kwenye kipindi cha Baragumu cha Channel Ten, Bi. Mnanka ameeleza kuwa vyama vya siasa vina wajibu wa kuweka mawakala wakati wa uchaguzi ambao jukumu lao ni kuhakikisha uchaguzi unaendeshwa kwa kuzingatia sheria.

Amesema mbali na mawakala wa vyama vya siasa, watazamaji wa uchaguzi wa ndani na wa nje na wagombea wanaruhusiwa kwa mujibu wa sheria kushuhudia upigaji kura ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa wazi na wa haki.

Tume inatarajia kushiriki kwenye vipindi kupitia vituo mbalimbali vya redio, televisheni na njia nyingine kutoa elimu ya mpiga kura kwa umma ili kuwaelimisha wapiga kura na wananchi kwa ujumla majukumu ya Tume na kujibu maswali yatakayoulizwa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatekeleza jukumu la kutoa Elimu ya Mpiga Kura kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, gari la matangazo la Tume, mitandao ya kijamii, mikutano na wadau wa uchaguzi, machapisho na kushiriki maonesho mbalimbali ambapo hukutana na wapiga kura ana kwa ana.

UNESCO yawapiga Msasa Watumishi 33 wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Na Mwandishi wetu

Watumishi 33 wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kati ya washiriki 5000 kutoka nchi 160 duniani ambao wanashiriki mafunzo ya uandishi wa habari kwa njia ya mtandao ambayo yameandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala sehemu ya Raslimali Watu Bw. Leonard Tumua, watumishi hao wanatoka Idara za Usimamizi wa Uchaguzi na Habari na Elimu ya Mpiga Kura ambapo lengo ni kuwawezesha watumishi hao kumudu changamoto za upashanaji habari za uchaguzi katika zama hizi za kidijitali.

Bw.Tumua amebainisha kuwa Wakurugenzi Wasaidizi wawili ambao ni Dkt Cosmas Mwaisobwa kutoka Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura na Bw.Kassim Sapi Mkwawa wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi ni miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo.

Mkurugenzi huyo Msaidizi amelishukuru Shirika la UNESCO kwa kuandaa mafunzo hayo kwani yatawawezesha watumishi wake kuzitambua na kuzikabili changamoto mbalimbali za kidijitali zikiwemo zile za mtandao, mitandao ya kijamii na jinsi akili bandia inavyoathiri michakato ya uchaguzi.

Mafunzo hayo yamegawanyika katika moduli tano ambapo kila wiki washiriki watajifunza moduli moja ambapo mada zilizoandaliwa katika mtindo wa video na maandishi huwekwa katika akaunti binafsi za kila

mshiriki na kufuatiwa na maswali matano ya chemsha bongo ambayo yanapaswa kujibiwa.

Mkufunzi Kiongozi kutoka Shirika la UNESCO Bi. Albertina Piterbarg ameeleza kuwa mafunzo hayo yameanza tarehe 19 septemba, 2022 na yanatarajiwa kuchukua wiki tano hadi tarehe 23 Oktoba, 2022 ndipo yatakamilika ambapo washiriki watakaofaulu watapatiwa vyeti.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV